**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA**

SHULE YA SEKONDARI
IWAMBI, S. L. P 2780,
**MBEYA**
.
SIMU MKUU: 0752196452
MAKAMU:0754256836
MTAALUMA:0785-551631
*Email: iwambiss@mbeyacc.go.tz*

*Kumb.Na. IWB/SS/MCC/KDT.1/2025/02* Tarehe ………………..

JINA LA MWANAFUNZI ……………………………………………………………………..

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI IWAMBI HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA MKOA WA MBEYA MWAKA ………………………**

**UTANGULIZI**

1.Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule ya sekondari Iwambi mwaka …………….. na utasoma tahasusi ya……………...

2.Shule yetu ipo umbali wa kilometa saba (07) magharibi mwa makao makuu ya jiji la Mbeya katika eneo la TAZARA – barabara kuu iendayo Tunduma.
Shule itafunguliwa rasmi **tarehe……………….**

3.Unatakiwa kuripoti shuleni bila kuchelewa kwa kufuata tarehe rasmi ya kufungua shule ukiwa na michango yote na tarehe ya mwisho wa kuripoti shuleni ni **…………………** vinginevyo utakuwa umepoteza nafasi hiyo adhimu.

**NB:** Endapo utahitaji mawasiliano zaidi tumia namba za simu na E-mail zilizopo hapo juu kulia.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

SARE ZA SHULE

**A. Wasichana**

1. Sketi mbili za **kijivu iliyokolea** (**isiyopauka**). Aidha, sketi zote mbili lazima zivuke magoti, kwa urefu usiopungua futi moja kushuka chini. (**Sketi zishonwe kwa mtindo wa Rinda box**)

2. Mashati mawili meupe ya tetroni mikono mirefu (blauzi). Mashati yawe marefu kuweza kuchomekea.
3. Jozi mbili za viatu vyeusi (siyo raba) vya kamba. Viatu visiwe na visigino virefu (ghorofa au soli nene kupita kiasi.
4. Soksi ndefu (stocking) nyeupe jozi mbili au zaidi.
5. Sweta rangi ya kijivu iliyokolea iwe na ''V *shape*'' sehemu ya shingo.
6. Raba nyeupe jozi moja na nguo za michezo; Tracksuit rangi ya kijivu iliyokolea na T-shirt nyeupe inayovaliwa siku ya ijumaa (siku nzima) na kwenye matukio ya michezo.
7. Tai mbili rangi ya kijivu iliyokolea

**B. Wavulana**

1. Suruali mbili za rangi ya **kijivu iliyokolea ( isiyopauka**). Aidha, suruali zote mbili lazima ziwe na marinda mawili au matatu sehemu ya mbele. (**Epuka suruali model**)
2. Mashati mawili meupe ya tetroni mikono mirefu. Mashati yawe marefu kuweza kuchomekea.
3. Jozi mbili za viatu vyeusi (siyo raba) vya kamba. Viatu visiwe na visigino virefu (ghorofa au soli nene kupita kiasi.
4. Soksi ndefu (stocking) nyeusi jozi mbili au zaidi.
5. Sweta rangi ya **kijivu iliyokolea** iwe na **''V *shape*''** sehemu ya shingo.
6. Raba nyeupe jozi moja na nguo za michezo ;Tracksuit rangi ya kijivu iliyokolea na T-shirt nyeupe.Huvaliwa siku ya ijumaa(Siku nzima) na kwenye matukio ya michezo.
7. **Mkanda mweusi wa ngozi** usio na maandishi/ picha/michoro.
8. Tai mbili rangi ya **kijivu iliyokolea**

**NB:**

1. Napenda kutahadharisha kuwa mzazi/mlezi yeyote ambaye atamnunulia mtoto wake sare isiyotakiwa atalazimika kununua sare nyingine. Sare itakaguliwa siku ya kuripoti shuleni. Unatakiwa uripoti shuleni ukiwa umevaa sare kamili ya shule.

2. **Mwanafunzi kula chakula shuleni ni lazima.Mahitaji ya chakula cha mchana kwa MUHULA MMOJA ni kama ifuatavyo;**

i)Mahindi yaliyokobolewa Debe moja.
ii)Maharage sado mbili (kilo kumi)
iii)Mchele sado moja
iv)Fedha Shilingi elfu ishirini(20,000) kwaajili ya malipo ya mpishi, ununuzi wa Viungo na mafuta ya kupikia pamoja na gharama ya nishati ya kupikia.

**Maelekezo zaidi yanapatikana kwa mwenyekiti wa kamati ya wazazi Mr.Mwasile 0767-751321.Au fika shuleni kwa ufafanuzi zaidi kutoka kamati ya wazazi.**

**MZAZI/MLEZI AHAKIKISHE ANAMPATIA MWANAYE MAHITAJI YAFUATAYO;-**

i) Madaftari makubwa yasiyopungua kumi na moja (counter books quire 3), madaftari madogo ya mazoezi kwa kila somo, kalamu ya wino na risasi na rula,
ii) Faili la plastiki
iii) Nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja na gharama ya matibabu (pale itakapohitajika).
iv) **Ream mbili** (A4)
v) Vitabu vya tahasusi ya masomo husika
vi) Ndoo moja ya lita ishirini
vii) Kwanja 1, jembe 1, reki 1,mopa 1, mifagio 2 wa ndani na nje
viii) Spring file moja kwaajili ya kuhifadhi nyaraka binafsi za mwanafu

**MICHANGO MBALIMBALI**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 35,000.00 |
| 2 | Tahadhari | 5,000.00 |
| 3 | Nembo | 5,000.00 |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000.00 |
| | **Jumla** | **50,000.00** |

**NB:Michango yote iliyopo kwenye jedwali ilipwe kwenye akaunti ya shule.Benki ya NMB namba 61001200140.Jina la akaunti ni: IWAMBI SECONDA SCHOOL**

**SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo. ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
(e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(f) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
(g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(h) Kutunza mali binafsi na mali za umma.
(i) Hurusiwi kubadili jina ulilojiandikisha shule ya msingi ulilofanyia mtihani wa Taifa isipokuwa kwa kibali maalumu cha Afisa Elimu wa Mkoa.
(j) Huruhusiwi kubadili dini/dhehebu bila kibali cha wazazi au walezi. Aidha, huruhusiwi kuendesha shughuli za dini/ibada mbali na vipindi maalumu vya dini vilivyowekwa katika ratiba ya shule.
(k) Huruhusiwi kujihusisha na masuala ya kisiasa au ushabiki wa kimichezo kinyume na maagizo ya shule.
(l) Huruhusiwi kujihusisha na udanganyifu wowote wa mitihani.
(m) Huruhusiwi kuchangia/kuchangisha fedha yoyote shuleni kinyume na maagizo/maelekezo ya serikali.

**MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUKUSABABISHIA KUSIMAMISHWA NA AU KUFUKUZWA SHULE**

i) Wizi
ii) Uasherati, mapenzi na ushoga.
iii) Ubakaji.
iv) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
v) Kupigana na kupiga.
vi) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
vii) Kudharau bendera na wimbo wa Taifa.
viii) Kuwa mjamzito/kupata mimba/kusababisha kupata ujauzito/mimba
ix) Kuoa au kuolewa.

x) Kutoa mimba.
xi) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
xii) Kukataa/kugomea adhabu kwa makusudi.
xiii) Kuwa na simu ya mkononi.
xiv) Kucheza kamali.
xv) Utoro.
xvi) Unywaji/utengenezaji/uuzaji wa pombe.
xvii) Kuchangisha fedha kinyume na maelekezo ya serikali.

**MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.**

(a) Fomu ya matibabu (medical examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali (**Iwe na risiti ya kielektroniki**). Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni. Fomu hii inapatikana shuleni.
(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai,ijazwe na mwanafunzi mwenyewe na kuwasilishwa shuleni.
(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.
(d) Mkataba wa malengo yanayotarajiwa kufikiwa ............. kati ya mwanafunzi ,mzazi, mlezi na mwalimu.
(e) Hati ya malipo ya michango mbalimbali iliyoainishwa kwenye jedwali(Bank pay in Slip)

Tafadhari soma kwa umakini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**MWISHO, NAKUKARIBISHA SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI IWAMBI.**

**……………………….**
**DEOGRATIUS MBIGI**
**MKUU WA SHULE**

**PRIME MINISTER'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MBEYA CIYT COUNCIL**

IWAMBI SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 2780,
**MBEYA.**

DATE…………………………………….
Ref: NO. IWS/ INST/2024/01.
TO: medical officer,
………………………………………………………………
P.O.BOX ……………………………………………..,
**……………………………………………………**

**PART A:**
Mr/Miss…………………………………………………………………………....................
..........……………………………………………………………………………………

Please examine the above named student as to his / her physical and mental fitness for a full time student in this school.

Thank you.

**PART B: CATEGORIES OF EXAMINATION:**

1. Hemoglobin ……………………………………………………………………
2. P.V bleeding …………………………………………………………………….
3. Blood pressure …………………………………………………………………
4. Urine for sugar …………………………………………………………………
5. Pregnancy test …………………………………………………………………
6. Stool for routine examination ……………………………………………
7. Asthma …………………………………………………………………………
8. Skin diseases……………………………………………………………………
9. Leprosy ………………………………………………………………………..
10. Epilepsy ……………………………………………………………………….
11. Pulmonary tuberculosis …………………………………………………
12. Neurosis ……………………………………………………………………..
13. Venereal diseases ……………………………………………………………
14. Other serious diseases …………………………………………………….

**PART C: MEDICAL VERTIFICATION:**

I have examined the above named student and consider that he/ she is physically and mentally fit/ is physically and mentally unfit for a full time student.

Thank you.

………………………………………………………………
Name and signature………………………………………………….

Designation
Date …………………………………………………..

**JAMHURI YA MUUNGANO WA**

**TANZANIA OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

***HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA***

**SHULE YA SEKONDARI IWAMBI**

**FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI NA MKATABA WAKE**

Mimi ni mwanafunzi……………………. niliyesoma katika shule ya msingi………………..na kuhitimu darasa la saba mwaka ……………..ninayeishi na mzazi/mlezi wangu aitwaye ………………………………wa kijiji/mtaa wa……………………...……………………….

Ninaahidi kwamba:

a) Sitashiriki katika migomo,fujo na aina yoyote ya makosa ya jinai

b) Nitatii sheria na kanuni zote za shule kama zilivyoainishwa katika kipengele na.3.0

c) Nitasoma kwa bidii na nidhamu ya hali ya juu kwa manufaa yangu,ndugu na serikali ka ujumla.

d) Nitahudhuria shuleni na darasani kama inavyopaswa

e) Nitaepuka tabia ambayo inavunja heshima ya uanafunzi wangu niwapo nje na ndani ya shule.

f) Nitafika shuleni kwa muda uliopangwa kwa wakati kulingana na kanunu na taratibu za shule.

Nakili kuwa maelezo haya nimeyasoma na kuyaelewa. Ninaahidi kwamba nitayatekeleza kama inavyopaswa.

JINA LA MWANAFUNZI …………………......…………………………………………………
KIDATO……………………………….…………………………………………..
MWAKA…………………………………….……………………….. ..........................

SAINI……………………………………….. …………………………………
TAREHE ……………………………………………………………………

**JAMHURI YA MUUNGANO WA**
**TANZANIA OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
***HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA***
**SHULE YA SEKONDARI IWAMBI**

**FOMU YA MZAZI/MLEZI**

Mimi………………………………….......................... Mzazi/Mlezi wa mwanafunza

.......................................................................................................................................

Anayeishi mtaa wa …………………………………………………………

a) Ninaahidi kwamba ninakubaliana na sheria, kanuni na taratibu za shule kama zilivyoainishwa kwenye fomu ya mwanangu.

b) Ninaahidi kuwa nitatoa ushirikiano kwa walimu na serikali kwa ujumla katika kuhakikisha kuwa mwanangu anahudhuria shuleni kama inavyopaswa.

c) Ninaahidi kuwa nitatoa mahitaji ya mwanangu ya shule kama inavyotakiwa

d) Nitahakikisha kuwa mwanangu anakuwa na nidhamu nzuri shuleni na nyumbani ili aweze kufanikiwa katika taaluma yake.

e) Nitahakikisha kuwa ninatimiza wajibu wangu kama mzazi/mlezi kwa kumtimizia mahitaji yake muhimu ya shuleni kama ilivyoagizwa.

JINA LA MZAZI/MLEZI …………………………………………………………
NAMBA YA SIMU …………………………………
SAINI …………………………………………
TAREHE …………………………….